

Ukuruzi wa 6, tarehe 28/01/2019

Habari

# Mpina awashushia rungu wapigaji sekta ya uvuvi

□ NA MWANDISHI MAALUM

**HATIMAYE** kibao kimewageukia wawekezaji waliokuwa wakijiingizia mamilioni ya fedha kila uchao kupitia shughuli za uvuvi kwenye hifadhi ya bahari huku 'wakitipiga' serikali kwa kutoilipa stahili yake.

Hali hiyo inatokana na amri ya serikali iliyowataka wawekezaji wote wenye kukabiliwa na madeni wawe wameyalipa yote ndani ya kipindi cha mwezi mmoja kuanzia sasa, kabla ya kuchukuliwa hatua kati za kisheria.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ndiye aliyetishia desturi hiyo ya wawekezaji kwenye Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU), kutoilipa serikali kwa kuwaambia wazi kuwa wasipomaliza madeni yao ambayo kwa ujumla yamefikia sh. milioni 331.2, kamwe serikali haitasita kuvunja mikataba yao na mwishowe kuwakamata wahusika, kutaifisha mali zao kwa nia ya kufidia mali za umma na kisha kuwafikisha mahakamani.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi jana, ilieleza kuwa Waziri Mpina alitoa agizo hilo wakati akizunguma katika ziara ya kutembelea Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu kwenye Visiwa vya Mbudya na Bongoyo, ambapo ilibainika kuwa baadhi ya wawekezaji waliopewa maeneo kwenye hifadhi hizo, wameshindwa kuyaendeleza kwa mujibu wa mikataba yao na pia kushindwa kulipa tozo stahili za serikali.

Waziri Mpina alisema kuwa serikali ya awamu ya tano kamwe haiwezi kukubali kuchezewa na wawekezaji ambao hawajajipanga na kuchelewesha uendelezaji wa fukwe na maeneo mengine ya urithi wa nchi na kukwamisha ukusanyaji wa mapato yake halali ambayo ndiyo hutumika kukamilisha shughuli mbalimbali za maendeleo.

Akieleza zaidi, Waziri Mpina alisema Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu ina

utajiri na urithi mkubwa wa nchi kwa sababu kuna fukwe ndefu na nzuri za kipekee duniani, makaburi yenye historia ya kuvutia, mazalia ya samaki, matumbawe yenye mvuto wa kipekee na ndege wa aina za kipekee, ambao baadhi hawapatikani katika maeneo mengine duniani.

Aidha, katika hatua nyingine, Waziri Mpina alisema pamoja na kuwapo kwa vivutio vingi vya kipekee, bado kitengo husika hakijavitangaza vivutio hivyo kikamilifu na mfano mmojawapo ni kwamba hadi sasa, hakuna mabango kwenye milango ya kuingilia nchini ikiwamo viwanja vya ndege,

**“Mtu mwingine yeyote, mwenye cheo chochote, akija kuwalaghai wananchi na kuwaambia uongo, tofauti na maelekezo ya sheria, mkamateni na ashtakiwe kama mhalifu mwingine na ninyi msimamo wenu uwe wa kisheria.”**

bandarini na mipakani.

Vilevile, alisema kuwa hakuna matangazo pia kwenye vyombo vya habari na matokeo yake, hilo linachangia wananchi wengi kutofahamu urithi huo na kwamba pia, hilo linachangia kuwapo kwa idadi ndogo ya watalii wa ndani na nje ya nchi wanaokwenda kutembelea hifadhi hizo.

Waziri Mpina aliagiza kuandaliwa mkakati wa kutangaza vivutio hivyo ili mwishowe visaidie kuvutia zaidi watalii na kukuza pato la taifa.

“Mkakati huo ufike wizarani kwangu Februari 28 mwaka huu,” alisema Waziri Mpina.

## KUTEGEMEA RUZUKU

**Wakati huohuo,** Waziri Mpina alielezea mshangao wake kwa kuona kuwa taasisi hiyo ikishindwa kujiendesha, badala yake kutegemea ruzuku ya serikali licha ya kuwapo fursa nyingi na vyanzo vingi vya mapato,

hivyo akatoa mwezi mmoja ili kuandaliwa kwa mkakati wa kuongeza ukusanyaji wa mapato na kuifanya taasisi hiyo kujitegemea kuanzia mwaka ujao wa fedha wa 2019/2020.

Pia, Waziri Mpina aliwataka watumishi wa taasisi hiyo kushikilia msimamo wa sheria iliyoanzisha taasisi yao na kwamba, kama kuna maelezo na mawazo ya kiseria, malalamiko hayo yawasilishwe kwa viongozi wakuu wa wizara.

“Mtu mwingine yeyote, mwenye cheo chochote, akija kuwalaghai wananchi na kuwaambia uongo, tofauti na maelekezo ya sheria, mkamateni na ashtakiwe kama mhalifu mwingine na ninyi msimamo wenu uwe wa kisheria,” alisisitiza Waziri Mpina

Meneja wa Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU), John Komakoma, alimhakikishia

Waziri Mpina kuwa, maagizo yote aliyoyotoa atayasimamia kikamilifu na kuona yanatekelezwa kwa wakati ili kuiwezesha taasisi yao kutoa mchango unaostahili kwa taifa.

Komakoma alisema ili kuleta ufanisi wa kazi, kitengo hicho kiko kwenye hatua ya mwisho ya mapitio ya Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Namba 29 ya mwaka 1994, ili kuiwezesha taasisi hiyo kuhifadhi maeneo tengefu yaliyoko kwenye mito mikubwa, mabwawa na maziwa kote nchini.

Pia, alisema katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018, kitengo hicho kimepokea watalii 45,000, ambapo kati ya hao, 26,000 ni watalii wa ndani na 19,000 ni watalii wa nje, hivyo kuingiza kiasi cha wastani wa sh. bilioni 1.6, kwa mwaka na wanatarajia kuwa na ongezeko kubwa zaidi la watalii katika kipindi cha mwaka huu wa fedha.